



KIBABII UNIVERSITY COLLEGE

UNIVERSITY EXAMINATIONS

**2014/2015 ACADEMIC YEAR
SECOND YEAR SECOND SEMESTER**

MAIN EXAMINATION

FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

COURSE CODE: KIS 207

**COURSE TITLE: THEORY AND PRACTICE OF TRANSLATION AND
INTERPRETATION IN KISWAHILI**

DATE: Monday 4th May 2015

TIME: 11:30am – 1:30pm

MAELEKEZO

Jibu maswali **matatu** pekee.

Swali la Kwanza ni la **lazima**

MUDA: Masaa Mawili (2)

KIBUCO observes **ZERO** tolerance to examinations cheating

Maswali

- 1 (a) Fafanua kwa muhtasari dhana ya tafsiri (ala 4)
(b) Eleza majukumu matatu ya tafsiri kwa jamii ya kisasa. (ala 6)
(c) Taaluma ya isimu-linganishi ni muhimu sana kwa mwana tafsiri. Dhihirisha. (ala 10)
(d). Tafsiri kauli zifuatazo kutoka kwa lugha chanzi hadi lugha pokezi ya Kiswahili. (alama 10)
- i. This is the house that Jack built.
 - ii. I expect them to arrive a week from next Friday.
 - iii. We all know that linguistics is an interesting subject.
 - iv. You are requested not to consume food in this establishment.
 - v. English is a language that is unique from other languages because of its unique roots.
- 2 Kwa kutumia mifano ifaayo, jadili sababu zozote *tano* zinazopelekea kuwepo kwa upungufu katika tafsiri. (alama 20)
- 3 Fafanua aina za tafsiri huku ukitoa mifano madhubuti kwa kila aina. (alama 20)
- 4 Aina mahususi ya matini ndiyo inayotumiwa kuamua mbinu mwafaka ya tafsiri. Ainisha matini ya tafsiri kwa kutumia kigezo vya *dhima ya lugha*. (alama 20)
- 5 Hakiki makala ya tafsiri ya habari uliyopewa. (alama 20)

Matini Chanzi: Kiingereza

The Secretary General of the United Nations Organization, Kofi Annan, fired one top official blaming him for failing to ensure the security of the officers of the organization. Mr. Annan also chastised a highly respected deputy, Ms. Louise Frechette of Canada, who submitted her resignation but Mr. Annan refused to accept it. The action yesterday appeared to be unprecedented in the United Nations Organization, where senior officers are almost never rebuked publicly for such an offence.

Kutoka: *The Daily Nation*, April 5th 2004.

Matini Lengwa: Kiswahili

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Kofi Annan, alimwachisha kazi kinara wake wa usalama akimlaumu kwa kushindwa kuhakikisha usalama wa maafisa wa u moja huo . Annan pia alimshutumu vikali naibu wake, Bi. Louise Frechette wa Canada, lakini alikataa ombi lake la kujiuzulu. Hii ni mara ya kwanza kinara wa umoja huo kuzomea waziwazi maafisa wake kwa kufuatia kosa kama hilo.

MWONGOZO WA KUTAHINI

1. (a) **Dhana ya tafsiri:** tafsiri inahusisha uhawilishaji wa ujumbe kutoka lugha moja – Lugha Chanzi (LC) hadi nyingine – Lugha Lengwa (LL). Mawazo yanayoshughulikiwa sharti yawe katika maandishi, na si vinginevyo. Mawazo (au ujumbe) kati ya lugha chanzi na lugha lengwa sharti ‘yalingane’.

Tuzo: Alama 4: Jibu lizingatie hoja zote muhimu ili alama zote zituzwe vinginevyo, kadiria

(b) Majukumu ya tafsiri:

- i. Tafsiri kama njia ya mawasiliano.
- ii. Tafsiri kama nyenzo ya kueneza utamaduni.
- iii. Tafsiri kama mbinu ya kujifunza lugha.
- iv. Tafsiri kama kiliwazo cha cha nafsi ya mfasiri.

Tuzo: Maelezo ya hoja zozote tatu (Alama 2 x hoja 3 = Alama 6)

(c) Umuhimu wa Isimu-linganishi kwa mwana tafsiri:

- i. Humsaidia mtafsiri kuzingatia uhusiano fulani baina ya lugha mbili kimtindo na kimuundo.
- ii. Kazi ya tafsiri ni kitendo cha kukutanisha lugha mbili hivyo basi humsaidia kulinganisha sarufi za lugha mbili.
- iii. Taaluma hii humsaidia mtafsiri kuelewa mifumo ya lugha mbalimbali na jinsi lugha hizo zinavyotumia zana zake za kiisimu kutolea taarifa mbalimbali.
- iv. Wajibu wa mtafsiri ni kutafuta visawe vya lugha asili katika lugha lengwa ufahamu wa isimu-linganisi husaidia uelewa wa mifumo ya maana za kimsingi pamoja na maumbo ya uwakilishaji wa maana za kimsingi za LC kwa visawe vya LL.

Tuzo: Hoja zielezwe kwa mifano faafu: Alama 2.5 x hoja 4 = Alama 10

(d) Tafsiri za kauli

- i. This is the house that Jack built.
Hii ndiyo nyumba iliyojengwa na Jack
Hii ndiyo nyumba aliyojenga Jack.
- ii. I expect them to arrive a week from next Friday
Ninawataraji kuwasili juma moja baada ya Ijumaa ijayo.
- iii. We all know that linguistics is an interesting subject.
Zote tunafahamu kwamba isimu ni somo la kupendeza.
- iv. You are requested not to consume food in this establishment.
Unaombwa/mnaombwa kutokula chakula katika mahali hapa.
- v. English is a language that is different from other languages because of its unique roots.

Lugha ya Kiingereza inatofautina na lugha nyingine kwa sababu ya asili yake ya kipee.

Tuzo: Alama 2 x Hoja 5 = Alama 10 (Zingatia ulinganifu kimaana)

2. Sababu zinazopelekea kuwepo kwa upungufu katika tafsiri:

a) Tofauti za Kiisimu:

-Maumbo ya Kiingereza huruhusu kauli elekezi kutoonyesha umoja au wingi wa wahusika, wakati wala majina ya vitu mahsusi vinavyoambatana na maelezo yanayotolewa. Kwa sababu hii, mfumo huu unaruhusu kutoa taarifa zilizo pana zaidi.

-Kiswahili kwa upande mwingine hulazimu kubainisha vipengele hivi vyote.

-Mifano:

Kiingereza

Kiswahili

No parking

Usiegeshe (gari hapa)

-Baadhi ya watafsiri hutumia miundo ya kisintaksia ya Kiingereza katika tafsiri za Kiswahili na hivyo kupelekea kupotosha maana. Kwa mfano:

Kiingereza

Kiswahili

A thousand time

elfu mara

b) Tofauti za mitindo ya lugha

Ingawa katika matumizi ya Kiswahili imeanza kujitokeza aina za mitindo, bado Kiswahili hakijawa na uwezo mkubwa wa kutofautisha mitindo mbalimbali iliyokwishajibainisha katika lugha zilizoendelea. Mifano:

Matini ya Kiingereza

Matini ya Kiswahili

Thou shalt not steal (Mtindo wa Kidini)

Usiibe

Do not steal (Mtindo wa Kawaida)

Usiibe

c) Tofauti za Kiitikadi

Taarifa nyingi zenye mwelekeo wa kisiasa tunazosisoma au kuzisikia kwenye vyombo mbalimbali vya habari daima huathiriwa na itikadi za watafsiri wake. Tazama mifano ifuatayo:

Neno *businessman* limetafsiriwa kuwa:

(i) Bepari, mlanguzi (Tafsiri inayoegemea itikadi ya ujamaa ya Tanzania, 1967 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1980)

(ii) Mfanyabiashara (Tafsiri inayoegemea itikadi ya sasa ya ubepari uchwara).

d) Tofauti za mila na mazingira

Tofauti za mazingira, mila na desturi baina ya watumiaji wa lugha chanzi na wale wa lugha lengwa mara nyingi hufanya tafsiri ama ziwe ngumu (na pengine kushidikana kabisa) ama ziwe pungufu katika maudhui yake. Mifano ni kama vile:

High tea (Kiingereza) ? (Kiswahili) Utamaduni wa Kiswahili hauna dhana hii.

Ice skating (Kiingereza) ?? (Kiswahili).

e) Tofauti za misemo, nahau, vitendawili na methali

kawaida misemo au tamathali za semi, nahau, mithali na vitendawili husukwa na kutumiwa kwa kufungamana sana na utamaduni wa watu fulani. Uchoraji wa dhana zinazowakilishwa na mafungu haya ya maneno sio tu hufanywa kwa usanii wa hali ya juu, bali pia desturi, imani, historia, mazingira na falsafa ya watumiaji wa lugha inayohusika.

f) Tofauti za Kifasihi.

Kila lugha huwa na sauti zake, huakisi utamaduni tofauti na huwa na matumizi ya zana anuwai za kiisimu katika kusuka maudhui ya kazi za kifasihi huwa ya namna ya kipekee. Kazi za aina hii si rahisi kutafsirika kwa ufanisi na ubora unaokubalika.

Sababu nyingine za upungufu katika tafsiri ni pamaoja na:

- Tofauti za Miundo ya Lugha
- Tofauti za Tamaduni
- Tofauti za Mitazamo ya Waandishi
- Tofauti za Historia

Tuzo: Ufafanuzi wa hoja zozote tano kwa mifano ifaayo: Alama 4 x Hoja 5 =Alama 20. Kadiria maelezo kabla kutuza alama zote.

3. Aina za tafsiri:

a) Tafsiri ya neno kwa neno.

- Maneno na mofimu hutafsiriwa pweke pweke kwa kuzingatia maana zake za kimsingi.
- Haizingatii matumizi ya neno kimuktadha.
- Mpangilio wa maneno na mofimu za lugha chanzi hubakia vilevile.
- Maneno yanayofungamana na utamaduni hutafsiriwa kisisisi. Mifano:

Kiswahili: a – li – lala hadi asubuhi

Kiingereza: *she/past/sleep/untill/morning*

Kiswahili: a – li – kwenda mpaka nyumbani kwake

Kiingereza: *she/past/go/untill/at/house/his*

Tafsiri Sisisi

Maneno hutafsiriwa pwekepweke kwa kuzingatia maana zake za msingi katika lugha chanzi.

Haizingatii muktadha muktadha wa matumizi ya lugha.

Haizingatii utamaduni wa lugha chanzi.

Aidha inakosa kutilia maanani hali za mawasiliano.

Hufuata mfumo wa kisarufi – sintaksia ya lugha lengwa.

Mifano:

Kiingereza: *Masanja was taken to the Central Police Station*

Kiswahili: Masanja alipelekwa kwenye Kituo cha Kati cha Polisi. (Badala ya Kituo Kikuu cha Polisi)

Kiingereza: *Dear listeners, lend me your ears.*

Kiswahili: wasikilizaji wapendwa, niazimeni masikio yenu. (Badala ya naomba mnisikilize)

b) **Tafsiri ya Kimawasiliano/ tafsiri fasaha.**

- Tafsiri ya kimawasiliano inamlenga mpokeaji wa matini lengwa/msomaji wa matini kwa kuamsha hisia zake kama ilivyo katika matini asilia.
- Mpokeaji wa makala husisitizwa ili ujumbe uliotafsiriwa umfikie.
- Tafsiri hii inampa mtafsiri uhuru wa kutafuta visawe vya nahau, methali, misemo, utamaduni na mazingira ya lugha lengwa.
- Hufuata miundo ya kisarufi ya lugha lengwa na inampa mfasiri nafasi kubwa ya kufasiri ujumbe.
- Mfasiri ana uhuru wa kuboresha mantiki ya matini chanzi na kusahihisha makala asilia ili afanikishe mawasiliano.

Mifano

Kiingereza: Good wine needs no bush.

Kiswahili: *Chema chajiuzza kibaya chajitembeza.*

d) **Tafsiri ya Kisemantiki/tafsiri maana**

Tafsiri hii huwasilisha ujumbe /maana katika miundo ya sarufi ya lugha pokezi.

Maana kamili ya ujumbe/matini chanzi husisitizwa.

Inazingatia maana ya neno kimuktadha – kwa jinsi lilivyotumika katika muktadha wa matini chanzi.

Inadhamiria kumpa mpokeaji maana iliyokusudiwa katika matini chanzi.

Mifano

Kiswahili: Alikwenda mpaka nyumbani kwake.

Kiingereza: *He went up to his home.*

Kiingereza: *Translation is criticised for its defects than praised for its merits.*

Kiswahili: Tafsiri hukosolewa kwa upungufu wake kuliko kusifiwa kwa faida zake.

Tuzo: Alama 5 x Hoja 4= Alama 20. Maelezo bila mifano yasituzwe zaidi ya alama 3/5.

4. Uainishaji wa matini kwa kigezo cha Dhima ya Lugha

Kulingana na Buhler (1965) lugha ina dhima kuu tatu:

- i). **Dhima Elezi:** ambapo lugha hutumiwa kwa madhumuni ya kueleza hisia za mtu binafsi bila kujali hadhira. Kiini cha dhima elezi ni mwandishi.
- ii). **Dhima Arifu:** ambapo lugha hutumiwa kama nyenzo ya kutolea taarifa. Kiini cha dhima arifu ni ukweli.
- iii). **Dhima Amili:** hapa lugha hutumiwa kwa madhumuni ya kuibua au kuchochea hisia za hadhira. Kiini cha dhima amili ni hadhira.

Kwa kufuata dhima kuu hizi za lugha, tunaweza kuainisha matini za aina tatu – matini elezi, matini arifu na matini amili.

1 Matini Elezi: Matini elezi huegemea zaidi kwa mwandishi. Mwandishi hutumia lugha kueleza hisia zake bila kujali jinsi

maelezo hayo yatakavyopokelewa na hadhira (wasomaji). Mifano ya matini elezi ni pamoja na:

- i). Fasihi iliyobuniwa kwa makini, kama vile ushairi, hadithi fupi, tamthiliya, riwaya n.k.
- ii). Kauli za kimamlaka au kimadaraka, kama vile hotuba na nyaraka za kisiasa, nyaraka za kisheria, kazi za kisayansi, kifalsafa na kitaaluma zilizoandikwa na wataalam walioboea.
- iii). Wasifu nafsi, insha, mawasiliano ya kibinafsi baina ya watu, hasa matini hizi zinapoandikwa kutokana na hisia za mwandishi binafsi bila kujali sana wasomaji lengwa.

2 Matini Arifu: Hizi ni matini zinazohusu mada yoyote ile ya maarifa, kwa mfano sayansi, teknolojia, biashara, uchumi, n.k. Kwa kawaida matini hizi huwa katika maumbo sanifu, mathalani vitabu, ripoti za kiufundi, makala katika magazeti au majarida ya kitaaluma, tasnifu, madondoo ya ajenda za mikutano au kumbukumbu za mikutano, n.k.

Matini arifu zina sifa kuu mbili:

- i). Matini hizi ndizo zinazotafsiriwa na idadi kubwa zaidi ya wafasiri walioajiriwa katika mashirika ya kimataifa, makampuni makubwa ya watu binafsi na asasi nyinginezo za tafsiri.
- ii). Asilimia kubwa ya matini hizi zimeandikwa vibaya na pengine huwa na taarifa tenge, zisizo na ukweli. Hivyo huwa ni jukumu la mtafsiri kufanya masahihisho yanayohitajika ya maudhui na mtindo wa lugha. Na ndiyo maana aghalabu tafsiri huonekana kuwa bora kuliko matini chanzi (au hutarajiwa ziwe hivyo).

3 Matini Amili: Matini amili zimeegemea zaidi upande wa hadhira (wasomaji). Matini hizi hulenga kuibua hisia za msomaji na kumfanya afikiri au atende kwa namna ambavyo imekusudiwa na matini mahususi. Mifano ya matini amili ni pamoja na matangazo, maelekezo, propaganda, maombi, mialiko, fasihi pendwa kama vile riwaya pendwa.

Kwa mujibu wa matini amili, yapo mambo mawili yanayopaswa kuzingatiwa:

- i). Uhusiano baina ya mwandishi na hadhira sharti uonyeshwe bayana kutokana na zana za kiiisimu zinazotumiwa. Kwa mfano, ofisa wa ngazi ya chini wizarani amwandikiapo waziri barua ya kumkwomba jambo fulani, basi hulazimika kutumia maneno kama vile:

Kwa mheshimiwa waziri

Kwa heshima na taadhima

- ii). Matini amili lazima ziandikwe katika lugha inayoeleweka kwa hadhira mara moja. Hadhira isipouelewa ujumbe uliomo kwenye matini, basi itakuwa muhali kwake kutekeleza matarajio ya mwandishi.

Tuzo: kueleza dhima za lugha= Alama 3

Kuainisha matini kwa kigezo hiki na kufafanua: Alama 5 x Hoja 3= Alama 15

Mifano faafu

= Alama 2

Jumla

= Alama 20

5. Uhakiki wa tafsiri:

Tafsiri hii imehamisha ujumbe muhimu lakini ikashindwa kuhifadhi maana kamilifu. Baadhi ya maana huonekana kupotea na zingine kupotoshwa. Tunabaini upungufu huu kwa kulinganisha baadhi ya kauli za matini hizi:

Kiingereza

Kiswahili

one top official

kinara wake wa Usalama

a highly respected deputy

naibu wake

submitted resignation

?

appeared unprecedented

ndio mara ya kwanza kinara ...

publicly

waziwazi

Kwanza, maana katika '*submitted resignation*' haionekani kushughulikiwa. Arifa katika kauli hii imetolewa kwa maana ya kushadidia uzito wa kitendo cha katibu mkuu wa Muungano wa Mataifa.

Pili, maana za kauli zingine zimepotoshwa ifuatavyo:

- Kauli ya '*one top official*' haina maana ya '*kinara wa usalama*'. Tafsiri hii imekiuka mipaka ya maana ya matini na kupotosha ujumbe.
- Maaana ya '*highly respected*' haikushughulikiwa. Tena matumizi ya kibainishi, {a}, ina maana ya kuwa kuna manaibu wengine, na si yule mmoja pekee.
- Kauli ya '*appeared unprecedented*' ina maana ya '*kuwezekana kuwa mwanzo*' na sio kuwa kwa uhakika unaosikika katika kauli '*hii ndio*'.
- Neno '*publicly*' halina maana ya '*waziwazi*' ila '*hadharani*'. Tendo linaweza kuwa waziwazi lakini pia faraghani.

Tuzo: Kubaini makosa/upungufu katika tafsiri: Alama 5

Kufafanua namna maana inavyopotoshwa: Alama 10

Kupendekeza namna upungufu huo unavyoweza kufidiwa: Alama 5

Jumla

Alama 20